

## **WENYEVITI WA MITAA WAELIMISHWA KUHUSU UMILIKI WA ARDHI YA MAENEO YA NDANI YA MANISPAA**

Wenyeviti wa Mitaa wa Manispaa ya Morogoro wameelimishwa kuhusu uuzaji wa ardhi kwenye mitaa kwamba unatakiwa kufanyika kwa kufuata sheria na taratibu za nchi.

Elimu hiyo yenye lengo la kupunguza wingi wa kesi za ardhi mahakamani imetolewa na ndugu Agustino Mtaki kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), katika kikao kati ya wenyeviti wa mitaa na Menejimenti ya Manispaa ya Morogoro, kilichofanyika leo tarehe 11 Agosti 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Manispaa hiyo.

Ndugu Agustino, amesema kwamba kwa mujibu wa sheria ya nchi yetu ya Tanzania, ardhi yote ya Manispaa, Miji na Makao Makuu ya Wilaya ni mali ya Kamishna wa Ardhi. Hivyo Mwenyekiti wa Mtaa wala mtu mwingine ye yote haruhusiwi kuyauza wala kusimamia uuzaji wake.

Aidha, ndugu Agustino ametoa wito kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro kuendelea kutoa elimu ya masuala ya ardhi ndani ya Manispaa ili kuwaokoa wananchi wake dhidi ya migogoro ya ardhi na kupunguza msongamano wa kesi za masuala ya ardhi mahakamani.

### **MWISHO**